# MWONGOZO WA KULINDA SHULE NA VYUO VIKUU KUTOKANA NA MATUMIZI YA KIJESHI WAKATI WA VITA

**Makundi yanayokabiliana wakati wa vita yanashauriwa kutotumia shule na vyuo vikuu kwa njia yoyote ile katika kuendeleza shughuli zao za kivita. Huku ikizingatiwa kwamba kuna uwezekano baadhi ya matumizi hayatakiuka sheria za kimatiafa zinazotumika wakati wa vita, kila mmoja wa makundi hasimu anashauriwa kujiepusha na hatua ambayo itahatarisha elimu na maisha ya wanafunzi, kwa kutumia vipengee vifuatavyo kama mwongozo:**

---

**Mwongozo wa 1:** Shule na vyuo vikuu ambavyo vinaendelea na shughuli zao za kielimu, hazifai kutumiwa kwa njia yoyote na makundi ya wapiganaji katika mgogoro wa kivita ili kuunga mkono juhudi zao za kivita.

(a) Mwongozo huu unahusu shule na vyuo vikuu ambavyo vimefungwa kwa muda nje ya wakati wa saa za kawaida za darasani, mwisho wa wiki, na siku kuu za mapumziko na pia wakati wa likizo.

(b) Wahusika katika migogoro ya kivita hawafai kutumia nguvu wala kutoa vishawishi kwa wasimamizi wa shule ili wawaondowe watu kutoka shule na vyuo vikuu kwa ajili ya kutumika kwa shughuli za kijeshi.

---

**Mwongozo wa 2:** Shule na vyuo vikuu ambapo watu wamehama au kuhamishwa kwa sababu ya hatari zinazotokana na migogoro ya kivita hazipaswi kutumiwa na makundi ya wapiganaji wa pande zinazohusika katika mgogoro wa kivita kwa madhumuni yoyote ya kuendeleza juhudi zao za kijeshi, isipokuwa katika hali isiyoepukika kwa kupunguza makali na ambapo hawana namna nyingine inayowezekana kati ya matumizi hayo ya shule au chuo kikuu, na mbinu nyingine inayoweza kutumika kuzipa pande zote mbili nguvu za kijeshi. Majengo mengine yanaweza kutumika badala ya majengo ya shule na vyuo vikuu, hata iwapo hayako katika eneo mwafaka au katika hali nzuri , isipokuwa wakati majengo hayo yanalindwa na sheria za Kimataifa kuhusu haki za kibinadamu (kwa mfano hospitali), na kwa kuzingatia kuwa pande zinazohusika katika mgogoro wa kivita lazima zichukue tahadhari zote zinazowezekana kuwalinda raia dhidi ya mashambulizi.

(a) Matumizi yoyote kama hayo ya shule au vyuo vikuu ambapo watu wamehama au kuhamishwa lazima yawe ya muda mfupi iwezekanavyo.

(b) Shule au vyuo vikuu ambapo watu wamehama au kuhamishwa na ambavyo vinatumiwa na vikosi vya pande zinazohusika katika mgogoro wa kivita kwa shughuli zao za kijeshi zinapaswa kuachwa wazi ili kuwawezesha wasimamizi wa elimu kuzifungua punde tu inapowezekana baada ya vikosi vya kivita kuondoka, ilmradi tu hali hii haitahatarisha usalama wa wanafunzi na wafanyakazi.

(c) Harakati au dalili zozote za kijeshi au kujihami kwa ajili ya kujizuia kijeshi lazima ziondolewe mara moja baada ya kuondoka kwa wapiganaji, huku kila juhudi zikifanywa kurekebisha uharibifu wowote wa miundomsingi ya taasisi hiyo. Hasa, silaha zote, zana na vilipuzi ambavyo havijalipuka au masalio ya zana nyingine za kivita lazima yaondolewe kutoka katika eneo hilo.

---

**Mwongozo wa 3:** Shule na vyuo vikuu havifai kamwe kuharibiwa kama hatua ya kuwanyima makundi hasimu katika mgogoro wa kivita uwezo wa kuvitumia katika siku za usoni. Shule na vyuo vikuu – viwe vimo katika shughuli zao za kawaida, au vimefungwa kwa muda au kwa ajili ya likizo, vimehamwa au watu kuhamishwa – ni maeneo ya kutumika na raia.

---

**Mwongozo wa 4:** Wakati wa mapigano kuna uwezekano kwamba wapiganaji wa pande husika katika mgogoro watashambulia majengo ya shule au vyuo vikuu. Hata hivyo makundi haya yanahimizwa kwamba kabla ya kutekeleza mashambulizi hayo, yanafaa kuzingatia njia nyingine, ikiwemo, kuwaonya maadui wao kwamba kuna kusudi la kutekelezwa shambulizi, ili waweze kuondoka mara moja au kusitisha shughuli zao mapema, isipokuwa katika hali isiyoruhusu.

(a) Kabla ya mashambulizi yoyote dhidi ya shule ambayo imelengwa kijeshi, pande zinazohusika katika mgogoro wa kivita sharti zizingatie kwamba watoto wana haki ya kuheshimiwa na kupewa ulinzi maalum. Jambo lingine muhimu la kutilia maanani ni athari za muda mrefu ambazo huenda zikajitokeza katika jamii katika juhudi zao kupata elimu kutokana na uharibifu wa au kuharibiwa kwa shule.

(b) Matumizi ya majengo ya shule au Vyuo vikuu na wapiganaji wa upande mmoja wa mgogoro wa kivita, hayapaswi kuwa shinikizo kwa kundi pinzani linaloteka maeneo hayo na kuendelea kuyatumia kwa shughuli zao za kijsehi. Harakati zozote za kijeshi na kuongezwa kwa wapiganaji au kujengwa kwa ngome za kijeshi zinafaa kusitishwa mara moja iwezekanavyo, na majengo na maeneo ya shule na vyuo vikuu kurejeshwa kwa umma kwa lengo la kutumiwa kwa jukumu la kielimu.

---

**Mwongozo wa 5:** Wapiganaji wa makundi yanayohusika katika mgogoro wa kivita wasiajiriwe kama walinzi katika shule na vyuo vikuu, isipokuwa pale ambapo njia nyingine za kutoa usalama hazipo. Ikiwezekana raia ambao wamepata mafunzo ya kutosha wanapaswa kutumika kutoa ulinzi katika shule na vyuo vikuu. Ikiwa kuna haja zaidi , basi itiliwe maanani , kuhamishwa kwa watoto, wanafunzi na wafanyakazi hadi eneo salama.

(a) Ikiwa vikosi vya wapiganaji vinashiriki katika kazi ya kutoa usalama kwa shule na vyuo vikuu, lazima kuwepo kwao katika eneo hilo au ndani ya majengo husika, kuepukwe ikiwezekana ili kuzuia hali ya kuvurugwa kwa hali ya kawaida ya uraia katika taasisi husika na kuvuruga mazingira ya kutolewa kwa elimu.

---

**Mwongozo wa 6:** Pande zote husika katika mgogoro wa kivita lazima, zishirikishe Mwongozo huu na vipengee vyake kwa mfano, imani zao, mafundisho ya kijeshi, sheria za ushiriki, na njia nyingine za kueneza habari, ili kuhimiza kutumika katika nyanja zote za kijeshi. Makundi yote husika katika mgogoro wa kivita yanafaa kuamua njia bora ya kufanya hivyo.